



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**  
**TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI**



**TAARIFA KWA UMMA**

**KUHUSU UTEUZI WA MBUNGE WA VITI MAALUM**

**Dodoma, 09 Julai, 2022**

Katika kikao chake cha tarehe 09 Julai, 2022, Tume ya Taifa ya Uchaguzi kwa kuzingatia matakwa ya ibara ya 78(4) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977 ikisomwa pamoja na kifungu cha 86A (6) na (8) cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343 imemteua Ndugu Tamima Haji Abass kuwa Mbunge wa Viti Maalum kwa tiketi ya Chama cha Mapinduzi.

Uteuzi huo umefanyika baada ya Tume kupokea barua ya tarehe 12 Mei, 2022, yenye Kumb. Na. CEB.137/400/02A/10 kutoka kwa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania iliyoandikwa kwa mujibu wa kifungu cha 37(3) cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343 ikiitarifu kuhusu uwepo wa nafasi wazi ya Mbunge wa Viti Maalum wa Chama cha Mapinduzi (CCM) kutokana na kifo cha aliyekuwa Mbunge wa Viti Maalum Mheshimiwa Irene Alex Ndyamkama.

Dkt. Wilson Mahera Charles

**MKURUGENZI WA UCHAGUZI**  
**TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI**